

**OFISI YA WAZIRI MKUU
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



BARAZA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI



**MKAKATI JUMUISHI WA KUENDELEZA UJASIRIAMALI
TANZANIA**

TOLEO FUPI

NOVEMBA, 2017

1. UTANGULIZI

Ujasiriamali – yaani kuanzisha na kuongoza mabadiliko ikiwemo kuanzisha na kukuza biashara¹ - ni muhimu katika kuendeleza ufanisi, ushindani na ukuaji wa uchumi. Malengo ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa, Dira ya Taifa ya Tanzania ya 2025, na sera zinazohusiana na maendeleo ya biashara ndogo na za kati, elimu, uwezesaji, maendeleo ya vijana na ajira zinatoea kipaumbele katika kuendeleza ujasiriamali ili kupata matokeo yaliyokusudiwa. Hata hivyo, utekelezaji wa mipango na sera hizi umekuwa si mzuri kutokana na kukosekana mwongozo makini wa utekelezaji. Mkakati jumuishi wa kuendeleza ujasiriamali unatoa dira na mwongozo wa kutekeleza mipango na sera hizi, ikiwemo hatua mahususi zinazohitaji kuchukuliwa, majukumu ya taasisi mbalimbali, uratibu na ufuatiliaji na tathmini ya juhudi za kuendeleza ujasiriamali.

Maandalizi ya mkakati huu yameshirikisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na ya binafsi, wakiwemo walengwa. Mkakati ni jumuishi kwa maana kwamba (i) unalenga kuleta matokeo kwa makundi yote muhimu – kuanzia maskini wanaojikimu, biashara zinazotumia ubunifu na teknolojia ya hali ya juu, biashara rasmi, wanawake, wanaume, wenye ulemavu, nk (ii) unazingatia nguzo kuu sita za kuendeleza ujasiriamali yaani utekelezaji makini wa mkakati, uboreshaji wa sheria zinazoathiri biashara, upatikanaji wa mitaji, elimu na stadi za ujasiriamali, matumizi ya teknolojia na ubunifu na uelewa na ushirikiano wa wadau.

2. DIRA, DHIMA NA MALENGO

Dira ni Kuwa na mtizamo na uwezo ulioimarika wa kijasiriamali unaopelekea upatikanaji wa ajira bora, ukuaji wa uchumi na hali bora ya maisha kwa wanawake, wanaume, vijana na makundi maalum.

Dhima ni Kujenga mfumo wa kuendeleza mtizamo na uwezo wa kijasiriamali unaowezesha kuanzisha na kukuza biashara na kukabili changamoto za maendeleo kwa njia bunifu na endelevu.

Lengo ni kutekeleza mkakati jumuishi kwa kuzingatia mahitaji ya kijamii na mazingira na kukabili vikwazo vya ushiriki sawa wa vijana, wanawake, wanaume, and wenye mahitaji maalum kwenye uchumi. Malengo mahususi kwa kila mhimili ni kama ifuatavyo:

Jedwali 1: Malengo mahususi kwa kila mhimili

¹ Kuendeleza ujasiriamali kwenye biashara kunajumuisha biashara zinazokua, bunifu na zinazotumia teknolojia na siyo tu zile zisizo rasmi au za kujikimu

Mhimili	Lengo
Kuboresha sheria na taratibu zinazosimamia biashara	Kupunguza vikwazo na gharama za kuanzisha na kuendesha biashara kwa kurahisisha sheria na taratibu, kuboresha miongozo kwa wafanyabiashara, kuboresha faida zitokanazo na kuendesha biashara rasmi na kuweka mazingira yanayotabirika ya kuanzishia biashara na kuheshimika kwa mikataba
Kuboresha upatikanaji wa elimu na stadi za kijasiriamali	Kutambua ujasiriamali kama somo rasmi kwenye shule na vyuo na kuhakikisha linafundishwa kwa wanafunzi wote na katika ngazi zote za elimu, na kuimarisha elimu isiyo rasmi hasa kwa kuendeleza kujifunza kwa vitendo
Kuwezesha upatikanaji na matumizi bora ya teknolojia na ubunifu	Kuendeleza ushirikiano kati ya sekta ya umma na ya binafsi ili kusambaza elimu, kuzidisha ushirikiano kati ya watafiti na biashara na hivyo kuzidisha ubunifu kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii, na kutumia tehamu katika kubuni na kuboresha huduma na mbinu za kufanya kazi
Kuboresha upatikanaji wa mitaji	Kubuni huduma za fedha zinazolenga mahitaji maalumu ya wajasiriamali na kuimarisha sekta ya fedha iwezeshe sekta binafsi kwa kutoa aina tofauti za huduma za kifedha kulingana na mahitaji na uwezo wa makundi tofauti
Kuboresha uelewa na ushirikiano miongoni mwa wadau	Kujenga utamaduni wa kijasiriamali, na kukabiliana na mitizamo hasi ya jamii na hasa ihusuyo wanawake, vijana na makundi yenye mahitaji maalumu. Kuboresha ushirikino na sekta binafsi, mitandao, kuaminiana miongoni wa wadau wanaohusika na kuendeleza ujasiriamali

3. HATUA ZITAKAZOCHUKULIWA KWA KILA MUHIMILI

3.1 – Kutekeleza Mkakati

Kuna sera kadhaa zinaonyesha umuhimu wa kuweka mazingira wezeshi ya kuendeleza ujasiriamali Tanzania. Ili sera hizi zilete matokeo yaliyokusudiwa, inabidi zitafsiiriwe kwenye vitendo na wadau mbalimbali huku kukiwa na ushirikiano, uratibu na tathmini. Zifuatazo ni hatua ambazo zitachukuliwa katika kuhakikisha utelekezaji makini wa mkakati jumuishi wa kuendeleza ujasiriamali:

Jedwali 2: Hatua zitakazochukuliwa kutekeleza mkakati wa kuendeleza ujasiriamali kwa umakini

Vikwazo	Hatua zinazopendekezwa
----------------	-------------------------------

Kukosekama uelewa wa pamoja wa dira ya kuendeleza ujasiriamali na pia kutokuwepo taratibu imara za kufanya tathmini ya maendeleo ya ujasiriamali	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha ripoti ya kila mwaka juu ya “Hali ya Ujasiriamali na Biashara Ndogo na za Kati Tanzania” kuonyesha ukuaji, afya ya sekta na maboresho yanayohitajika. • Kufanya kampeni za kuongeza uelewa wa Mkakati wa Kuendeleza Ujasiriamali na Mpango Kazi Wake • Kufanya tathmini za mara kwa mara za hali ya ujasiriamali nchini • Kutangaza matokeo ya utafiti uliofanywa na UNCTAD na Baraza la Uwezeshaji (NEEC) juu ya hali ya mfumo wa uendelezaji ujasiriamali Tanzania (2016) • Kufanya utafiti unaoitwa “Global Entrepreneurship Monitor (GEM) hapa Tanzania kwa ushirikiano na taasisi ya GEM
Kukosekana kwa sheria inayosimamia maendeleo ya ujasiriamali na biashara ndogo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha sheria ya kuendeleza ujasiriamali na biashara ndogo na za kati • Kuimarisha uwezo wa Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Uendelezaji Ujasiriamali
Kukosekana kwa mifumo ya kuratibu juhusi za kuendeleza ujasiriamali	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha muundo na utendaji wa Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) na majukwaa mengine ya majadiliano kati ya sekta binafsi na ya umma • Kuanzisha majukwaa ya sekta binafsi kufuatilia na kutoa msukumo utekelezaji wa Mkakati wa kuendeleza ujasiriamali
Kutokuwepo tathmini na kujifunza vya kutosha kutokana na hatua na mbinu zinazotumika kuendeleza ujasiriamali	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaa viashiria na mifumo ya ukusanyaji taarifa kuhusu utekelezaji na matokeo ya sera za ujasiriamali • Kufanya tathmini ya athari na mambo tunayojifunza kutokana na mbinu mbalimbali zinazotumika kuendeleza ujasiriamali

2.2 – Kuboresha sheria na kanuni zinazosimamia biashara

Ili uwezo wa kijasiriamali uweze kutumika na matokeo yake kuonekana, inabidi kuwe na mazingira ya biashara kuanzishwa, kuendeshwa na kukuzwa kisheria na kwa njia nyepesi na isiyokuwa na gharama kubwa. Pamoja na juhudi mbalimbali ambazo zimeshafanyika kuboresha mazingira ya biashara Tanzania, bado kuna vikwazo na changamoto nyingi za kisheria kama ambavyo zimeorodheshwa kwenye jedali namba 3.

Jendwali Na 3: Hatua za kuchukua kuboresha sheria na kanunu zinazosimamia biashara

Kikwazo	Hatua za kuchukua
Kukosekana utaratibu mahususi wa	<ul style="list-style-type: none"> • Kulinganisha gharama na muda unaotumika kuanzisha biashara rasmi katika serikali za mtaa mbalimbali • Kuanzisha utaratibu wa kisheria wa kuchambua kwa mapana athari

kuchambua mchakato na gharama za kuanzisha biashara	<p>za mabadiliko ya sera na sheria kwa biashara kabla hazijapitishwa</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kushawishi upande wa serikali kuheshimu majukwa ya kujadiliana na sekta binafsi katika ngazi ya wilaya, mkoa, sekta na taifa
Mchakato mrefu na gharama kubwa za kuandikisha biashara na kupata leseni	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha na kurahisisha taratibu za kuandikisha, kutoa liseni na kulipa kodi ikiwemo kuboresha matumizi ya mtandao. • Kutekeleza kwa ukamilifu na makini Mpango wa Kuboresha Sheria na Kanuni za Biashara (Blueprint on business regulatory licensing reforms) • Kuanzisha vituo vya huduma (One Stop Centres) kwenye serikali za mitaa kuweka taratibu za uandikishaji na utoaji liseni pamoja
Kutofautiana taratibu na kukosekama uwazi na miongozo katika ulipaji kodi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuondoa utaratibu wa kulipa kodi ya mapato kabla ya kuanza biashara • Kuanzisha utaratibu wa kusuluisha migogoro ya kibiashara ambao unaweza kutumiwa na biashara ndogo na za kati • Kuanzisha utaratibu wa kutoa elimu kuhusu haki miliki na utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa njia ya usuluishi
Kutokuwepo utaratibu wa kisheria na kikanuni unaotekelezeka na biashara ndogo kabisa (Zaidi ya asilimia 90 ya biashara zote) ambazo haziwezi kurasimishika kwa utaratibu wa kawaida	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha utaratibu wa kutoa elimu ya kuandikisha, kupata leseni na kutimiza masharti mengine ya kisheria ya kuendesha biashara kwa kutumia mtandao • Kuanzisha sera maalumu kutoa vivutio kwa biashara kurasimishwa • Kuanzisha mfumo maalumu wa kisheria kwa ajili ya kurasimisha biashara ambazo hazijafikia kiwango cha kupata liseni ya kawaida • Kuimarisha Madawati ya Uwezeshaji kwenye halmashauri za Wilaya

2.3 – Kuboresha upatikanaji wa elimu ya ujasiriamali na stadi za kuendesha biashara

Dira ya Taifa ya 2025, sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya 2004, Sera ya Maendeleo ya Vijana ya 2007, Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Sera ya Ajira ya 2008 na Sera ya Maendeleo ya Biashara Ndogo na za Kati ya 2003 zinasitiza haja ya kuingiza elimu ya ujasiriamali kwenye mitaala ya shule ya vyo na kutoa elimu na stadi za biashara nje ya vyo. Ili kufikiwa lengo la sera hizi maeneo yafuatayo bado yanahitaji kufanyiwa kazi:

Jedwali Na 4: Hatua za kuboresha utoaji wa elimu ya ujasiriamali na stadi za kuendesha biashara

Vikwazo	Hatua zinazopendekezwa
Kutokueleweka vizuri kwa nafasi ya elimu rasmi katika kuendeleza ujasiriamali na kukosekana kwa elimu ya vitendo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua mitaala na utoaji wa elimu ya ujasiriamali shuleni, vyuoni na nje ya mfumo rasmi na kuchukua hatua kuondoa mapungufu yaliyopo • Kuhamasisha vyuo kubadilika kwenda kizazi cha tatu cha utoaji elimu - kujumuisha ujasiriamali, ubunifu na kutatua matatizo, ikiwemo kufundisha kwa vitendo • Kuhimiza jamii, familia, waajirii, shule na vyo kuwa na utaratibu wa kutambua na kutoa tuzo kwa wale wanaoonyesha tabia za kijasiriamali na utayari kwa kutatua matatizo • Kuandaa nyenzo za kufundishia na kujifunzia ujasiriamali zinazofaa kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali
Upungufu wa watoaji bora wa huduma za biashara na wafanyabiashara kutokuwa tayari kulipia huduma hizi	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua idadi, upatikanaji, uwezo na mapungufu miongoni mwa watoaji huduma za kuendeleza biashara na kuanzisha utaratibu wa kusimamia ubora wa huduma zao • Kuhamasisha na kuwezesha uanzishaji wa utoaji elimu ya ujasiriamali kwa mtandao
Upungufu wa wawezeshaji mahiri wa elimu ya ujasiriamali na kukosekana kwa vivutio vya walimu kutumia wajasiriamali kufundisha	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha na kutekeleza program ya kujenga uwezo wa wawezeshaji wa ujasiriamali ikiwemo kutumia mifumo ya ILO-SIYB, UNCTAD- Empretec, na Kaizen, etc • Kutoa motisha kwa walimu wa ujasiriamali kutumia ufundishaji wa vitendo na kuwahusisha wanafunzi kwenye biashara • Kuanzisha mitandao wa watoaji elimu ya ujasiriamali waweze kushirikisha mbinu, nyenzo na uzoefu
Ushirikiano mdogo kati ya wafanya biashara ndogo na za kati na watoaji mafunzo ya ujasiriamali	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhimiza shule na vyuo kutumia wajasiriamali kuwatia moyo na kuwafundisha wanafunzi • Kuanzisha utaratibu wa kuwajengea wanafunzi na wahitimu uzoefu kwa njia ya kujitolea na ushauri kutoka kwa wafanyabiashara waliofanikiwa

2.4 –Kuwezesha matumizi ya teknolojia na ubunifu

Ni muhimu kwa biashara ndogo na za kati kutumia teknolojia na ubunifu kuboresha ufanisi, kupata huduma, kujifunza, kushirikiana na wadau wengine duniani kushindana na kukuza biashara. Hapa Tanzania, taasisi kama Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) zinatoa huduma muhimu katika kutekeleza sera za taifa kwa kuendesha viitamizi na vituo vya kuendeleza ubunifu. Changamoto ambazo bado zipo na hatua zinazopendekezwa kuzikabili zimeorodheshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali Na 5: Hatua za kuwezesha matumizi zaidi ya teknolojia na ubunifu

Vikwazo	Hatua zinazopendekezwa
Upungufu wa raslimali watu na uwezo wa kitaasisi wa uendelezaji teknolojia na ubunifu	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha mafunzo ya tehamu kwa watumishi wa umma. • Kutafuta raslimali za kuwekeza kwenye vituo vya kuendeleza ubunifu • Kuandaa na kutekeleza program za kujenga uwezo wa taasisi za utafiti na uvumbuzi.
Kukosekana vipaumbele na mipango maalumu wa kuendeleza utafiti na ubunifu na kuunganisha biashara ndogo na za kati kwenye milolongo ya thamani	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha na kupanua mipango ya kuunganisha biashara ndogo na makampuni makubwa. • Kuboresha uelewa wa ubunifu kwa njia mbalimbali kama maonesho, mitandao ya kijamii, warsha, machapisho. • Kuanzisha na kupanua mfumo wa ubunifu na ujasiriamali kwa kuanzisha na kuboresha viitamishi, science parks, maabara za ubunifu, hackathons - shuleni, vyuoni na kwa jamii kwa kutoa ardhi, fedha na motisha • Kuhimiza matumizi ya fungani (clusters) zinazoshirikisha taasisi za mafunzo na za utafiti katika kujifunza na kuboresha huduma, stadi, bidhaa, na kwa ujumla kutatua matatizo mbalimbali
Kutokuwepo mikakati na vivutio vya kujenga ushirikiano kati ya watafiti na biashara	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha majukwaa ya ubunifu yanayojumuisha serikali kuu, serikali za mitaa, watafiti na sekta binafsi. • Kupitia majukumu, miundo, na raslimali zilizomo kwenye taasisi za utafiti, teknolojia kwa jicho la kivumbuzi ili kuziboresha ikiwemo kuongeza ushirikiano kati ya watafiti, serikali na sekta ya uzalishaji • Kuweka motisha kwa watafiti, serikali na sekta binafsi kushirikiana katika kukabili changamoto na matatizo mbalimbali
Kukosekana program za kuunganisha utafiti na uanzishwaji biashara bunifu, na za kuchochea ushirikiano katika ubunifu miongoni mwa	<ul style="list-style-type: none"> • Kuanzisha utaratibu wa kufuatilia na kutathmini matokeo ya huduma zitolewazo kwa biashara • Kuweka vivutio vya ubunifu unaoshirikisha nchi za jirani na kwa kampuni zilizofanikiwa kuwekeza katika ubunifu • Kutangaza ubunifu unaoleta manufaa kwa watoto wa kike, wavulana na wanawake kupitia vyombo vya habari na njia nyinginezo

nchi jirani	
-------------	--

2.5 Kuboresha upatikanaji wa mitaji

Mfumo wezeshi wa kuendeleza ujasiriamali unapaswa uwezeshe upatikanaji wa mitaji ya aina mbalimbali kwa biashara za aina mbalimbali na kwa masharti ambayo yanawezekana kwa hayo makundi, kuchochea ubunifu, kupatikana kwa biashara zinazoanza, kuimarisha ukopaji na ukopeshwaji endelevu. Kwa Tanzania, bado kuna vikwazo vingi katika mfumo wa upatikanaji mitaji, kama ilivyoorodheshwa hapa chini.

Jendwali Na 6: Hatua za kuboresha upatikanaji wa mitajo

Vikwazo	Hatua zinazopendekezwa
Kutokuwepo huduma za fedha stahiki kwa baadhi ya mahitaji ya biashara ndogo na za kati, biashara zinazoanza na za hasa za vijana	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhamasisha na kutoa motisha kwa mabanki kuanzisha mikopo maalum ya kuanzisha biashara kwa vijana wa kike na kiume kama sehemu ya kuwajibika kwa jamii (CSR) • Kutumia tehamu na simu za mikononi kuwezesha biashara ndogo na wakazi wa vijijini kupata huduma za fedha. • Kuzitaka benki zitoe taarifa ya mikopo kwa makundi la wakopaji (ukubwa, jinsi, umri)
Kutokuwepo mifuko inayoshirikisha sekta ya umma na ya binafsi kwa ajili ya kutoa mitaji kwa ajili ya biashara bunifu, zinazotumia teknolojia mpya na zile zinazokua haraka sana	<ul style="list-style-type: none"> • Kutoa motisha kwa wanaonunua hisa kwenye biashara ndogo na za kati • Kuanzisha program za kujengea mabanki uwezo kuhudumia biashara mpya, ndogo na za kati • Kuanzisha mashindano na tuzo zitakazosaidia wabunifu vijana kutafisi ubunifu wao kuwa biashara
Biashara nyingi ndogo kutokuwa na dhamana na kukosekana kwa usimamizi dhabiti wa vyama vya kuweka na kukopa na taasisi nyingine za fedha	<ul style="list-style-type: none"> • Kukamilisha sheria ya taasisi za fedha ambazo hazisimamiwi na benki kuu • Kuharakisha utoaji wa vitambulisho ya kitaifa kwa wafanya biashara na kuunganisha takwimu za taasisi mbalimbali (NIDA, TRA, nk) • Kutekeleza mipango ya kutoa hati za kimila za umiliki ardhi kwa watu weng • Kuingiza taasisi zinazotoa mikopo ambazo hazisimamiwi na Benki Kuu kwenye utaratibu wa kupeana taarifa za wakopaji (credit reference bureaux)
Elimu ya fedha miongoni wa wafanya	<ul style="list-style-type: none"> • Kuharakisha utekelezaji wa National Financial Education Framework • Kufanya kampeni za kubadilisha mitizamo na tabia kuhusu ukopaji wa

biashara ndogo na kati kuwa mdogo na kusababisha taasisi za fedha kukosa Imani nao	busara na urejeshaji wa mikopo <ul style="list-style-type: none"> • Kujenga uwezo wa taasisi zinazotoa huduma zisizo za kifedha kutoa mafunzo ya uzimamizi wa fedha na ya kuandaa michanganuo • Kuboresha sheria ili kuwalinda wakopeshaji na wakopaji kwa usawa
--	--

2.6 –Kuboresha uwelewa na ushirikiano

Mfumo wa uendelezaji ujasiriamali unapaswa kujenga uelewa wa umuhimu wa ujasiriamali kwa jamii, kuonyesha fursa za kijasiriamali hasa zinazoweza kutumiwa kirahisi na vijana, kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza ujasiriamali na kuimarisha mitandao na ushirikiano. Yafuatayo ni maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi, na hatua zilizopendekezwa kuchukuliwa.

Jedwali Na 7: Hatua za kuboresha uelewa na ushirikiano

Vikwazo	Hatua zilizopendekezwa
Juhudi ndogo za serikali katika kutangaza umuhimu wa ujasiriamali na kauli zinazokinzana kuhusu thamani ya wajasiriamali katika jamii	<ul style="list-style-type: none"> • Kushiriki katika matukio yanayovumisha ujasiriamali mfano- Siku ya Kimataifa ya Ujasiriamali na kuanza kusheherekea Wiki na Siku ya Ujasiriamali Kifaifa. • Kuandaa mkakati wa mawasiliano kwa wizara na taasisi za serikali ili kujenga uelewa unaofanana na mtizamo unaothamini ujasiriamali • Kuandaa vivutio na tuzo mbalimbali kwa ajili ya kuchochea mabadiliko na mtizamo na tabia kuanzia ngazi ya familia hadi ya taifa
Kukosekana kwa taarifa kuhusu fursa za kijasiriamali, hasa zile zinazoweza kutumiwa na wahitimu wa shule na vyuo	<ul style="list-style-type: none"> • Kuchambua fursa za kijasiriamali zilizoko ambazo zinaweza kutumiwa kirahisi na vijana kuanza safari ya kijasiriamali bila kuhitaji fedha au ujuzi mkubwa • Kuimarisha Kamati ya Kitaifa ya Kuendeleza Ujasiriamali • Kuchambua kiwango na jinsi wanaomaliza vyuo wanavyojijiri ili kupata mwongozo wa kisera utakaoweka mazingira wezeshi zaidi
Sekta binafsi kutoshiriki kikamilifu kwenye juhudi za kuendeleza ujasiriamali.	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha ushirikiano miongoni mwa vyama na mitandao ya wajasiriamali na watoaji huduma kwa biashara kuanzia mahali wanapofanyia biashara. • Kuweka utaratibu wa kuwezesha sekta binafsi kushiriki kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza ujasiriamali kupitia kushirikiana na kujengeana uwezo wa ushawishi na utetezi • Kujenga uwezo na miundo inayoweza vyama vya wafanyabiashara kushiriki katika kuboresha sera, sheria, na huduma za biashara • Kuhamasisha uanzishwaji wa mitandao ya wawekezaji wanaonunua hisa na kulelea biashara ndogo na za kati (Angel Investors Networks) • Kujenga uwezo wa vikundi na mitandao ya vijana wajasiriamali ili waweze kupaza sauti yao katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara zao

2.7 – Hatua maalumu kuwezesha uwezesaji jumuishi

Kuendeleza ujasiriamali inatambulika kama njia muhimu ya kuleta maendeleo shirikishi. Ujasiriamali unaweza kujumuisha makundi yanayoishi kwenye mazingira magumu katika maendeleo. Ili kuwajumuisha vijana, wanawake, wenye ulemavu, maskini wa vijijini na makundi mengine yaliyoachwa nyuma katika maendeleo, hatua zifuatazo zitachukuliwa kuondoa vikwazo vinavyoyarudisha makundi haya nyuma kijasiriamali:

Jedwali Na 8: Hatua maalumu kujumuisha makundi maalum katika maendeleo ya ujasiriamali

Mhimili	Vikwazo	Hatua zinazopendekezwa
Kutekeleza Mkakati wa Kijasiriamali	Kukosekama sheria maalum kusimamia ujasiriamali jamii	Kuanzisha sheria ya Ujasiriamali Jamii (Social entrepreneurship) kuwezesha mifumo ya kibiashara ya kutoa huduma kwa biashara kustawi
	Hakuna majukwaa ya vijana wajasiriamali kujadiliana na serikali na hivyo sauti ya vijana haisikiki	Kuhamasisha vyama vya wafanyabiashara kuanzisha idara za vijana
Kuboresha sheria na kanuni za biashara	Kutokuwepo kwa njia maalumu za kutoa mwongozo kwa vijana wanaoanza au kuendesha biashara	Kuwezesha na kutumia maofisa wa vijana kwenye serikali za mitaa kuwaongoza na kuwashauri vijana wajasiriamali
	Kukosekana na vivutio vya biashara kuwa rasmi	Kuweka vivutio vya kurasimisha biashara vikilenga Zaidi vijana na akina mama
Kuboresha elimu na stadi za kijasiriamali	Kukosekana kwa nyenzo za kujifunzia na kufundishia ujasiriamali jamii	Kuandaa nyenzo za kufundishia na kujifunzia ujasiriamali jamii
	Kutokuwepo program za mafunzo zinazolenga vijana wajasiriamali	Kuandaa nyenzo za kufundishia na kujifunzia ujasiriamali kwa vijana
		Kuhamasisha matumizi ya burudani (edutainment) katika ufundishaji ujasiriamali
		Kuwezesha mbinu za kujifunza katika jamii (community learning)
Kuboresha uelewa na ushirikiano	Nchi ya Tanzania haiwatumii wajasiriamali waliofanikiwa kama mifano na kuwatia moyo wenzao	Kuhamasisha vijana kuanzisha na kuendeleza vyama vya kijasiriamali popote walipo na kuvijengea uwezo

5. UTEKELEZAJI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Hatua zilizoainishwa ni sehemu ya majukumu ya idara, wizara na taasisi za serikali na zisizo

za serikali. Kila moja kati ya idara, wizara na taasisi hizi inategemewa kupanga, kujipanga, kutafuta raslimali, kutekeleza na kufuatilia na kutathmini matokeo katika maeneo yanayoihusu. Uongozi wa utekelezaji utakuwa chini ya taasisi zilizoonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo.

Jedwali 9: Watekelezaji wa Mkakati kwa kila Mhimili

Eneo/Mhimili	Taasisi Kiongozi	Taasisi Nyingine
Uongozi na uratibu kitaifa	Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi NEEC/ Ofisiya Waziri Mkuu/PMO	TPSF
Kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Ujasiriamali	Wizara ya Fedha na Mipango (MFEA)	MITI, MoFEA SIDO, TPSF, MCDGC, TGNP, etc
Kuboresha sheria na kanuni	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (MITI)	TPSF, TCCIA, TBS, TFDA, GS1, TRA, OSHA, etc
Kuboresha elimu ya ujasiriamali na stadi za kuendesha biashara	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (MITI)	MITI, TCCIA, TIE, MoEST, VETA, NEEC
Kuboresha upatikanaji wa mitaji	Wizara ya Fedha na Mipango (MFEA)	BOT, TBA, TAMFI, COBAT, TIB Dvlp, TFBDSP, etc
Kuboresha matumizi ya teknolojia na ubunifu	Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)	R&DI, UDIEC, SUGECO, Incubators and labs, CAWAT, etc
Kuboresha uelewa na ushirikiano	Mamlaka ya Uendelezaji Biashara (TANTRADE)	PMOLEY, TAYOA, TFBDSP

Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi - NEEC – itakuwa ndiye kiongozi wa kuratibu na kufuatilia na kutathmini katika ngazi ya taifa. Kamati ya Mkakati Jumuishi wa Kuendeleza Ujasiriamali, inayosimamiwa na NEEC itakutana kila nusu mwaka kufuatilia utekelezaji na kutafuta njia za kukabili vikwazo vinavyokwaza utekelezaji. Kutakuwa na kamati ndogo kwa kila mhimili ambayo itakutana mara moja kwa kila robo mwaka kufanya kazi hiyo hiyo na kutoa taarifa kwa Kamati ya kitaifa inayokutana mara mbili kwa mwaka.

Vifuatavyo ndio viashiria vya mafanikio katika kila mhimili:

Jedwali Na 9: Viashiria vya Mafanikio kwa kila Mhimili

Mhimili	Viashiria
Kutekeleza Mkakati wa Kifaifa Kuendeleza	<ol style="list-style-type: none"> 1) Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Utekelezaji itakuwa imeundwa na inakutana walau mara 2 kwa mwaka kuanzia 2018 2) Walau tathmini moja ya kina itakuwa imefanyika ifikapo Disemba 2019 3) Ripoti ya Hali ya Ujasiriamali itatolewa kila mwaka kuanzia 2019 4) Utafiti wa kupima hali ya ujasiriamali Tanzania (GEM Survey)

Ujasiriamali	utafanyika Tanzania kuanzia 2020
Kuboresha sheria na kanuni za biashara	<ol style="list-style-type: none"> 5) Sheria za kusimamia ujasiriamali jamii, biashara ndogo sana na bishara ndogo na za kati itakuwepo ifikapo 2019 6) Asilimia ya biashara zisizo rasmi itashuka kutoka 89% hadi 70% au chini yake ifikapo 2021 7) Kutakuwepo utaratibu mwepesi wa kurasimisha bishara ambazo haziwezi kuingia kwenye utaratibu wa kawaida wa liseni ifikapo 2020 8) Gharama za kupata liseni na kutimiza masharti ya uendeshaji biashara zitapungua kwa walau 20% ifikapo 2021
Kuboresha elimu ya ujasiriamali na stadi za kuendeleza biashara	<ol style="list-style-type: none"> 1) Ujasiriamali utakuwa unafundishwa/unajifunzwa kwenye shule zote ifikapo 2021 2) Ujasiriamali unafundishwa kama somo kwa walau nusu ya wanafunzi wa vyuo vyote ifikapo 2021 3) Idadi wa wakufunzi waliofuzu kutumia mifumo ya kufundishia wajasiriamali ya Kaizen, SIYB, Empretec itaongezeka kutoka chini ya 10 hadi walau 50 ifikapo 2021 4) Mtaala wa mafunzo ya watoa huduma kwa biashara (BDS) utakuwa umeanza kufundishwa ifikapo 2021
Kuendeleza matumizi ya teknolojia na ubunifu	<ol style="list-style-type: none"> 1) Walau biashara 20 zinazotokana na utafiti kwenye vyuo na taasisi za utafiti kuwa zimeanzishwa ifikapo 2021 2) Walau vituo 50 vya ubunifu na ama uatamizi vitakuwa vinafanya kazi ifikapo 2021 3) Walau miradi 50 ya kuendeleza ubunifu itakuwa imegharamiwa na sekta binafsi ifikapo 2021 4) Walau 20% ya wahadhiri wa elimu ya juu watakuwa wanahusika kwenye shughuli za utafiti na ubunifu kwa ushirikiano na serikali au sekta binafsi ifikapo 2021
Kuboresha upatikanaji wa mitaji	<ol style="list-style-type: none"> 1) Walau mifuko 5 ya kuendeleza ubunifu itakuwa imeanzishwa ifikapo 2021 2) Walau mifuko 5 ya kuanzisha au kuendelea biashara bunifu za vijana iyakuwa imeanzishwa ifikapo 2021 3) Walau vijana wa kike 10,000 wakakuwa wamefaidika na mifuko ya kuendeleza ubunifu ifikapo 2021 4) Walau sheria tatu zinazolenga kuboresha upatikanaji wa mitaji kwa vijana na zitakuwa zimetungwa ama kuboreshwa ifikapo 2021
Kuboresha uelewa na ushirikiano	<ol style="list-style-type: none"> 1) Walau 50% nusu ya wadau wanaoendeleza ujasiriamali wanaufahamu mkakakati jumuishi wa kuendeleza ujasiriamali ifikapo 2021 2) Walau shule, vyuo, na jamii 500 zitakuwa zimeanzisha vyama vya ujasiriamali ifikapo 2021 3) Matamshi na vitendo vya watumishi wa serikali na wanasiasa vitakuwa vina akisi uelewa wa maana na thamani ya ujasiriamali ifikapo 2021

